

HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



NGHL/DC/63/182/55

26/03/2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale anawatangazia Waombaji wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi ya kazi ifuatayo;

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – (NAFASI 26)

Ngazi ya Mshahara ni TGS B sawa na Shilingi 390,000/= kwa mwezi.

1) SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya **Astahada/Cheti (TECHNICIAN CERTIFICATE NTA-LEVEL 5)** katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote Kinachotambuliwa na Serikali.

2) KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III

- a) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- b) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Kusimamia Utawala bora katika Kijiji.
- c) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- d) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- e) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria, na Taratibu.
- f) Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa Kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- g) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalamu katika Kijiji.

- h) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- i) Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- j) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- k) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na,
- l) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

3) MASHARTI KWA UJUMLA.

- m) Mwombaji awe ni Mtanzania asiezidi umri wa miaka 45 awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale.
- n) Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi Umma
- o) Mwombaji aambatanishe taarifa zake binafsi (CV) ikionyesha sanduku la posta, E-mail, namba za simu anazotumia na uzoefu wake kazini.
- p) Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha nne (IV) au sita (VI), cheti cha kuzaliwa na Picha 2 (passport size) za hivi karibuni.
- q) Mwombaji anatakiwa aambatanishe Vyeti vilivyo sainiwa na kupigwa muhuri (CERTIFIED COPY) wa Mwanasheria au Mahakama.
- r) Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **09/04/2018** saa **9:30** alasiri aidha maombi yote yawasilishwe kwa Anuani lfuatayo;.


Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 352,

HALMASHAURI YA WILAYA,

NYANG'HWALE.

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri www.nyanghwaledc.go.tz na katika mbao za matangazo.


Carlos K. Gwamagobe

Mkurugenzi Mtendaji (W)

NYANG'HWALE

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NYANG'HWALE

S. L. P. 352